# NAJUA

Bila shaka sisi ni watu wenye majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo, kuwa hai duniani, kuona wakati mwingine mkuu wa Pasaka. Pasaka daima huleta ki—kitu kitukufu sana kwetu, matumaini mapya. Na—na jinsi ilivyo kuu!

2 Na wakati nilipoingia tu chumbani huko nyuma asubuhi ya leo, mtu fulani alikutana nami na kusema, "Ndugu Branham, unamjua yu—yule mtoto mchanga, ama mtoto mdogo au mtu fulani, aliyeombewa huko Chautauqua mwaka jana, ambaye alipaswa kuondolewa moyo wake, na mishipa ya damu au kitu fulani kurekebishwa kwake." Kasema, "Mtoto huyo aliponywa, na yuko jengoni asubuhi ya leo, kwa kweli, na ameketi hapa asubuhi ya leo." Basi hilo ni sawa, tutakuwa na ushuhuda mfupi kutoka kwake labda kabla tu ya kuingia katika ibada nyingine. Na sisi ni watu wenye furaha kabisa.

3 Sasa nitamwomba Ndugu Neville kama atapata somo la Maandiko la Mathayo ama Luka, moja, juu ya ufufuo, iwapo hujalisoma tayari. Umelisoma, ndugu? [Ndugu Neville anasema, "La."—Mh.] Basi, tunapojiandaa kwa ajili ya maombi.

4 Na sasa inayofuata ibada hii, itakuwa ni ibada ya uponyaji. Ibada hii itakapomalizika, basi mtaenda kwenye kiamshakinywa chenu. Halafu, baada ya hapo, tutarudi tena mnamo saa tatu u nusu na kuanza ibada nyingine. Ndipo basi ibada za uponyaji zitafuata hiyo. Na kisha ibada za ubatizo zitafuata hiyo.

5 Na ni wakati mzuri jinsi gani kwa ubatizo! Loo, jamani! Ufufuo! Hiyo ndiyo sababu tunabatizwa, kwa sababu kwamba Yeye alifufuka tena.

6 Ninakumbuka kabla ya kuwa na mahali petu pa ubatizo hapa, nilikuwa nikiwapeleka mtoni hapa chini, mapema, asubuhi baridi zenye ukungu, na kuwabatiza watu huko chini kwenye mto. Kuna jambo fulani kulihusu ambalo, kabisa, ni wakati adhimu. Pasaka, ni wakati mkuu.

Nilikuwa nikimtazama Ndugu Pat Tyler akiketi hapa.

7 Nilikuwa tu nikizungumza na mtu jana usiku. Kwamba, mkutano wetu wa mwisho huko Oklahoma, nilijaribu, ninajaribu sasa (na nitatangaza hili) kuweka kando mpaka Mungu atakaponiita kuifanya, huduma yangu ya kale ya utambuzi, kwa sababu nafikiri (mwanzo) ni hu—huduma mpya inaingia.

8 Hivi majuzi usiku, bila mtu yeyote kujua chochote juu yake, niliijaribu juu ya mtoto aliyekuja jukwaani, alikuwa amezaliwa kipofu, mtoto mchanga; na alikuwa kipofu kabisa, mvulana

wa yapata umri wa miaka kumi na sita. Na mara ghafla akapiga mayowe, "Ndugu Branham, ninaweza kuona!" Na hapo, naye Pat alikuwa. . .Ty-. . .amesimama karibu, karibu sana na mvulana huyo, macho yake yalipofunguka kwa mara ya kwanza katika maisha yake yote. Na basi ninatumaini kwamba upo hapa na matarajio makubwa, pamoja nami, ninatazamia kitu fulani, Mungu atufanyie, na kutupandisha juu katika kiwango kingine kuliko kile ambacho tumekuwa.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

9 Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, kama tulivyokusanyika asubuhi ya leo, hapa katika kanisa hili dogo kando ya barabara, tuna shukrani tele kwa ajili Yako, kwa ajili ya yote haya yanayomaanisha kwetu, na hasa sana kwenye asubuhi hii ya Pasaka. Kama hakungekuwa na Pasaka, tusingekuwa katika hali tuliyomo leo. Hiyo, Pasaka ndiyo iliyotia muhuri ahadi zote za Mungu. Ilizithibitisha kwetu. Kila kitu ambacho Yeye aliwahi kuahidi, vyote vilifanywa halisi kwenye Pasaka. Moja ya siku kuu kuliko zote za sherehe tuwezayo kuwa nayo katika mwaka! Nasi tungeomba, Bwana, leo hii, kwamba Wewe utaifariji mioyo yetu tunapoketi, tukingojea, na chini ya matarajio kwa ajili ya Roho Mtakatifu, Yule aliyekuja baada ya Pasaka, aje juu ya mioyo yetu na kutufariji, na kuirejesha imani yetu, katika viwango vikuu vyenye nguvu, ili tuweze kutembea maisha yale ambayo Yesu alitukusudia kutembea.

10 Tungeomba kwa ajili ya kila mtu binafsi, na hasa sana kwa ajili ya wale ambao wamefungiwa ndani na wasioweza kufika kwenye ibada mahali popote leo hii. Mungu, uwe pamoja nao. Pia jalia—jalia Pasaka hii ilete Pasaka halisi kwao, kuinuka kutoka kitandani, na afya mpya ambayo hawajawahi kuijua hapo kabla maishani. Tujalie, Bwana.

11 Jalia kila mhubiri, kila mtumishi uliye naye kote ulimwenguni leo hii, ambaye anaadhimisha kumbukumbu hii kuu, jalia wawe na upako na nguvu na Uwezo, kuletea makusanyiko yao (kondoo wanaongojea) Chakula ambacho Mungu ameweka akiba kwa ajili ya watu Wake. Tujalie, Bwana. Tunangojea sehemu yetu, kwa unyenyekevu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

12 Nitamwomba Ndugu Neville atusomee Maandiko ya ufufuo. [Ndugu Neville anasema, "Mathayo 28," na anasoma Maandiko yafuatayo—Mh.]

> [*Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.*]
>
> [*Na, tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jiwe akalikalia.*]

[*Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji.*]

[*Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu.*]

[*Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa.*]

[*Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa Bwana.*]

[*Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia.*]

[*Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari.*]

[*Na walipoenda kuwaambia wanafunzi wake, tazama, Yesu akakutana nao, akisema, Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia.*]

[*Kisha Yesu akawaambia, Msiogope; enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.*]

[*Nao wale walipokuwa wakienda, tazama, baadhi ya askari waliingia mjini, wakawapasha wakuu wa makuhani habari za mambo yote yaliyotendeka.*]

[*Wakakusanyika pamoja na wazee, wakafanya shauri, wakawapa askari fedha nyingi,*]

[*Wakisema, Semeni, ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba,* hao *walipokuwa wamelala.*]

[*Na neno hili likisikilikana kwa liwali, sisi tutasema naye, nanyi tutawaondolea wasiwasi.*]

[*Basi wakazitwaa zile fedha, wakafanya kama walivyofundishwa. Na neno hilo likaenea kati ya Wayahudi hata leo.*]

[*Na wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu.*]

[*Nao walipomwona, walimsujudia; lakini baadhi yao waliona shaka.*]

[*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*]

[*Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;*]

[*na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na, tazama, nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina.* Sehemu tupu kwenye kanda.]

13 . . . aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

14 Sasa tungesema, kutangaza tena sasa, kwamba ibada, na kwa ajili ya asubuhi, zitaendelea mnamo saa tatu u nusu, punde tu tukitoka kwenye hii, ninii . . . ibada hii ya asubuhi sasa. Ndipo basi tunaiita hii ibada yetu ya mapambazuko. Pia sisi, tuna mambo fulani makuu ya kuwaripotia kuhusu mi—mikutano iliyopita. Pia tunataka ninyi mlio wagonjwa na mnaoteseka, ninyi nyote, mje kwa imani asubuhi ya leo, kuamini ya kwamba huyu Yesu aliyefufuka yuaishi leo, na Yeye ni yule yule tu kama alivyowahi kuwa. Hajabadilika hata kidogo.

15 Sasa ninataka kusoma sehemu ndogo ya Maandiko hapa, inayopatikana katika mlango wa 19 wa Ayubu, kuanzia kifungu cha 15.

*Wakaao nyumbani* mwangu, . . . *na vijakazi wangu, wanihesabu kuwa mgeni; Mimi ni mgeni machoni pao.*

*Namwita mtumishi wangu, wala haniitikii, Ingawa namsihi kwa kinywa changu.*

*Pumzi zangu ni kama za mgeni kwa mke wangu, ingawa nasihi kwa ajili ya watoto wa* mwili *wangu mwenyewe.*

*Naam, hata watoto wadogo hunidharau; Nikiondoka, huninena.*

*Wasiri wangu wote wanichukia; Na hao niliowapenda wamenigeukia.*

Mifupa *yangu inagandamana na ngozi yangu na nyama yangu, Nami nimeokoka na ngozi ya meno yangu tu.*

*Nihurumieni, nihurumieni, Enyi rafiki zangu, Kwa maana mkono wa Mungu umenigusa.*

*Mbona ninyi mnaniudhi kama Mungu, wala hamkutosheka na nyama yangu?*

*Laiti maneno yangu yangeandikwa* sasa*! Laiti* yangeandikwa *kitabuni!*

*Yakachorwa katika mwamba milele, kwa kalamu ya chuma na risasi.*

*Lakini mimi najua . . . Mtetezi wangu yu hai, Na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi.*

*Na ingawa baada ya . . . mabuu ya ngozi* kuuharibu *mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.*

*Nami nitamwona mimi nafsi yangu,. . .macho yangu yatamtazama, wala si mwingine, ingawa viuno vyangu viangamizwe ndani yangu.*

16 Ningependa kuchukua kwa ajili ya kifungu hapo, kinachopatikana katika hii Ayubu 19. *Najua*.

17 Yule mzee kwenye wakati huu alikuwa kwa namna fulani kama tulivyo leo hii. Alikuwa katika shida kubwa, kama tunavyoiita, "upeo wa matatizo," naye alikuwa anadhikika. Siku nyingi angeketi juu ya lundo la majivu, na alikuwa anajaribu kutafuta maneno ya kumfariji, akijaribu kutafuta kitu cha kumpa ujasiri, na kitu fulani ambacho kingekuwa—kingekuwa faraja kwake kwa kuwa aliona maisha yake yakififia.

18 Kwanza kabisa, alikuwa ni mtu mkongwe, yapata umri wa miaka tisini, naye alikuwa amecharazwa na mkono wa Mungu. Sasa, tunajua ya kwamba Mungu hakuwa amemgusa kwa mkono Wake, bali kwamba Mungu alikuwa amemkubalia Shetani kumgusa. Mungu anao tu mawakala kufanya mambo. Mungu akitaka uovu ufanywe, Yeye humwachilia tu Shetani kuufanya. Na kama akitaka wema ufanywe, Yeye anao watumishi Wake ambao Yeye huwaachilia kuufanya.

19 Naye Shetani alikuwa amemgusa Ayubu kwa kusudi, kumjaribu, kwa sababu yeye na Mungu walikuwa wamefanya mjadala. Ndipo Mungu akamwambia Shetani kwamba, "Ninaye mtumishi duniani, hakuna aliye kama yeye. Lolote nimwambialo, yeye atalifanya. Yeye ni mtu mkamilifu, na mtu mwenye haki."

20 Naye Shetani akasema, "Iwapo utanirushusu tu kumshika, nitamfanya akulaani usoni Pako."

21 Ayubu, bila ya kujua mambo haya yote yanayoendelea, ilimwingiza mzee huyo katika dhiki kubwa. Hata hivyo, kwa njia fulani, wakati wote walipomwacha, angali alishikilia mahali pake katika—katika Kristo. "Ninajua Mtetezi wangu yu hai," alisema.

22 Sasa tunafikia sehemu hizo. Sote tunafikia. Nami ninaamini kwamba leo, kwamba tumekusanyika hapa kwa ajili ya kitu kama kusudi lilo hilo. Sisi sote tuko kwenye lundo la majivu. Tuna matatizo yetu, na mema na mabaya yetu, na nyakati zetu za—za shida, na magonjwa yetu, na huzuni zetu, na masikitiko yetu. Kwa hiyo tunakuja hivi, asubuhi, asubuhi hii ya Pasaka, kupata maneno ya faraja, kama vile Ayubu alivyokuwa akijaribu kutafuta kutoka kwa rafiki zake.

23 Hakuna mmoja wao angaliweza kumpa faraja yoyote. Kwa sababu ya shida yake, walikuwa wakimshutumu kuwa ni mtenda dhambi kisiri. Ndipo, katikati ya matatizo yote, Mungu akaja kumwokoa.

24 Ayubu alikuwa akiuliza swali. Kama alivyojua, si kwamba alikuwa tu mgonjwa na majipu yake, na matatizo na huzuni, kutokana na kuipoteza familia yake na mali yake yote, alikuwa karibu kuchukua uhai wake; bali alikuwa ni mtu mkongwe, mwenye umri mkubwa, huku akijua kwamba alikuwa anaelekea kaburini. Na, akijua hivyo, aliamini ya kwamba kulikuwa na mtu fulani aliyemleta duniani, asingeweza kuja tu hapa mwenyewe. Basi alijua kwamba alitokana na baba na mama, bali, hata hivyo, huyo baba na mama ilibidi wawe na mtu fulani kuwaleta. Na ingezunguka irudi kwenye asili, "Ni nani aliyemleta wa kwanza, mmoja?"

25 Ndipo akashangaa hili. "Ni jambo la ajabu kwamba mimi hapa, ninatembea huku, maisha ya juu kuliko mnyama, na maisha ya juu kuliko maisha ya mimea." Lakini hata hivyo tunakuta ya kwamba alisema, "Mti ukifa, utaishi tena. Na kama u—ua likifa, litaishi tena." Lakini akasema, "Mwanadamu hulala chini, hukata roho, naye yuko wapi? Wanawe huja kumwomboleza na kutoa heshima, wala yeye hatambui." Naye alikuwa anashangaa, "Shida ilikuwa nini hata—hata Mungu angeuacha uhai wa namna hiyo kuishi tena, kama vile maua na mimea, bali mwanadamu asingeweza kuishi tena?" Haya yote yalimtatiza.

26 Na laiti tungechukua tu kutokana na hitimisho hili asubuhi ya leo. Na hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Tumeisikia hadithi ya Pasaka, tena na tena, na kuisoma huku na huku; na leo hii, katika matangazo yenu ya redio, mtawasikia wahudumu mbalimbali wakiiendea. Lakini kile nilichofikiria, kwa ajili ya kundi langu dogo asubuhi ya leo, Bwana amenipa, ningeliendelea kutoka kwa msimamo tofauti kama ningeweza, nikikaribia mahali pa: Kwa nini tunafikia shida hizi? Ni kitu gani kinachofanya mambo haya kutukia? Ni kwa nini Mkristo afadhaike kamwe? Ni kwa nini kila kitu, kisiende sawa tu kwa Mkristo? Bali hakiendi, na tunajua hivyo.

27 Na wakati mwingine tuna shida nyingi zaidi tunapokuwa Mkristo kuliko tulivyokuwa nazo tulipokuwa wenye dhambi. Hakika, imeandikwa, "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote." Mungu aliahidi mateso mengi, hisia za ajabu, na mambo ya ajabu ambayo yangepita ufahamu wetu, lakini daima hufanywa kwa wema wetu. Hatuwezi tu kuelewa, kwa sababu, kama tungeelewa, basi isingekuwa imani kwetu; tungetembea na ufahamu. Bali tunatembea, na tunayo, na tunaamini kwa imani, Neno Lake, kwamba litatufanyia jambo jema. Laiti tungalielewa hilo leo hii, asu—asubuhi hii. Kama tungalielewa kwamba shida zetu zote. . . Wala hakuna mmoja wetu asiyeweza kudhurika nazo. Na laiti tungaliweza kutambua kwamba mambo hayo ni kwa ajili ya wema kwetu!

28 Imeandikwa, katika mojawapo ya Maandiko katika Biblia, kwamba, "Majaribu yanayoletwa kwetu, yana thamani zaidi

kwetu kuliko dhahabu yenyewe, kwa kuwa ni Mungu anayetupa majaribu haya." Baada ya sisi kuwa mali yake, maungamo yetu na ubatizo wetu, na ahadi yetu kutembea maishani kwa ajili Yake, basi kila jaribu linalotujia ni kutukamilisha kwa ajili ya utukufu Wake. Ni la kutuleta mahali ambapo Mungu anaweza kujifanya Mwenyewe halisi zaidi kwetu kuliko alivyokuwa kabla ya jaribu kuja.

29 Ninataka kuungana asubuhi ya leo na Ayubu, kusema ya kwamba nimeishi muda mrefu kutosha kujua kuwa hiyo ni Kweli. Nimeiona katika maisha yangu mwenyewe, kwamba kila mara hali ngumu inapoinuka, ambayo siwezi kuizunguka, ama kupita chini yake au juu yake, Mungu hufanya njia, na hutokea kwa utukufu. Nashangaa tu jinsi neema Yake huifanya kamwe, bali Yeye huifanya.

30 Pia kumbukeni, katika mambo haya yote, Shetani hujaribu kutufadhaisha, na kutuhangaisha, kutufanya tufikirie, "Loo, mbona *hili* lilitendeka? Ni kwa nini singeweza kuwa *hivi*?"

31 Siku chache zilizopita nilipotoka mahali pazuri sana na penye mapambo kuliko pote nilipowahi kuona maishani mwangu mwote, lilikuwa ni jengo kuu la ndugu yetu, Oral Roberts. Nilipoona ile marmar tupu, na hakuna dirisha popote ndani yake, bali jinsi lilivyojengwa! Nami nimekuwa Hollywood na nimekuwa katika ikulu za wafalme, na nimekuwa kila mahali ambapo ningeweza, karibu, kote ulimwenguni, na mahali na nyumba maridadi, za kupendeza, bali sijawahi kuona chochote, mahali popote, pa kulinganisha, nalo, mahali popote hata kidogo. Jinsi ambavyo nyaya ndogo za alumini zimefunga pamoja u—upande wa ndani, na, loo, sijawahi kuona chochote maridadi hivyo maishani mwangu mwote. Nilipotembea kupitia pale, na kuchukua mikono yangu na kusugua nguzo hizo za miimo, na—na matale makubwa; yote katika mfano wa utatu wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, mi—michongo yake. Vitu hivyo vyote! Nilikuwa ndio kwanza nitoke kwa Ndugu Tommy Osborn, na kuona kazi yake kubwa mno huko kwa ajili ya Bwana.

32 Nilisimama nje, nikatazama jengo hilo, nikawazia, "Mungu, hakika nimekuwa mnafiki, hakika nimekuwa mtu aliyetengwa na jamii, mahali fulani; kwa kuwa, huduma za watu hawa zilitokana na yangu." Ndipo nikawazia, "Kitu gani? Labda siaminiki kabisa, Bwana, hata usingeniamini na chochote kama hicho. Hata maskini dola chache, ambazo Wewe hunijalia kulipa kwa ajili ya miamsho na kadhalika, sasa wanajaribu kunipeleka gerezani kwa sababu yake. Basi ni kwa nini mimi ni mnafiki hivi, ama ni kwa nini mimi ni mtu asiyeaminika hivi?"

Nilikuwa kwenye lundo la majivu, kama alivyokuwa Ayubu wa kale.

33 Niliposimama pale nje, karibu nisingeweza kupumua, kutokana na ukuu huo; kwamba maskini mvulana aliyezaliwa katika handaki, Mpentekoste, angeweza kufanya na kuleta hilo katika jengo hilo kubwa mno. Ndipo nikawazia, "Ee Mungu, labda mimi sistahili."

34 Wakati huo huo tu Sauti ndogo ikashuka kupitia vichochoro hivyo, na kusema, "Lakini mimi ndimi urithi wako."

35 Ndipo nikawazia, "Ee Bwana Mungu, loo, jalia hilo libakie tu hivyo, basi, Bwana. Mimi . . . kwa sababu nisingekuwa na akili kuendeleza kazi kubwa hivyo kwa ajili Yako. Na mimi ni m—mtu asiye na elimu. Lakini, mradi tu Wewe ni urithi wangu, mimi ni Wako, na Wewe utaniongoza. Nisingeweza kujiongoza mwenyewe. Lakini, Ee Bwana, niongoze!"

36 Ni saa hizo muhimu sana zinazotusukuma kwenye eneo takatifu. Ilikuwa katika Biblia. Basi kumbuka, haijalishi dhiki ni kubwa jinsi gani, Shetani hawezi kuondoa uhai wako mpaka Mungu amemaliza na wewe. Hakuna kitu kinachoweza kukufanyikia isipokuwa Mungu akiruhusu. Hakuna uovu uwezao kuja isipokuwa Mungu auruhusu. Na Yeye anafanya hayo kwa ajili ya wema wako. Hebu tuwazie.

37 Pale wakati gharika ilipokuja kuangamiza ulimwengu, haingeweza kumwangamiza Nuhu. Nuhu asingeweza kuangamizwa, kwa sababu kwamba Mungu alikuwa na kazi kwake kufanya.

38 Siku moja, katika taifa kuu chini ya utumwa mkuu, kulikuwa na watoto fulani wa Kiebrania ambao tunawafahamu kama Shadraka na Meshaki na Abednego. Ikafikia mahali ambapo iliwabidi kufanya uamuzi, kwamba jambo fulani ilibidi kufanywa. Walikuwa na . . . Imani ya—ya—yao ilijaribiwa.

39 Na wakati imani yako inapojaribiwa, basi usishindwe. Dumu moja kwa moja na kile unachoamini.

40 Basi wakati imani yao ilipojaribiwa. Ndipo wakaingia katika wakati muhimu. Hawakuenda tu kwenye lu—lundo la majivu, bali waliingia katika tanuri la moto. Lakini Shetani asingeweza kuwaangamiza, kwa kuwa kusudi la Mungu halikuwa limetimia bado. Wangeweza kuingia mle wakiwa na tumaini hili, "Najua Mtetezi wangu yu hai!" Wangeweza kuingia mle wakiwa na tumaini hili, "Tumehakikishiwa ya kwamba Mungu anaweza kutuokoa na tanuri hili la moto, bali, hata hivyo, hatutasujudia sanamu."

41 Shetani asingeweza kuwachukua. Hangeweza kumzamisha Nuhu katika gharika, mpaka kusudi la Mungu lilipokamilika. Hangeweza kuwateketeza wana wa Kiebrania, mpaka kusudi la Mungu lilipokamilika. Hangeweza kumwua Ayubu kwa majipu na matatizo, mpaka kusudi la Mungu lilipokamilika. Wala simba kuweza kumla Danieli, mpaka kusudi la Mungu lilipokamilika.

Wala mauti na uzee kuweza kumchukua Ibrahimu, mpaka kusudi la Mungu lilipokamilika.

42 Wala haiwezi kukuchukua, au kunichukua mimi, mpaka kusudi la Mungu, la maisha yetu, limekamilika. Hivyo basi, tunachukua kutoka hapo, faraja.

43 Basi ni kwa nini Mungu huachilia matatizo kuja? Mungu hulifunga nira tatizo, huweka lijamu kinywani mwake na kulifanya limtii Yeye, na matatizo hayo hutuleta katika ushirika wa karibu na Mungu.

44 Hakukuwahi kuwa na upinde wa mvua mpaka gharika ilipokuja. Lakini baada ya Nuhu kufinyiliwa katika hali hiyo aliyokuwemo, kuelea siku arobaini usiku na mchana, katika dhoruba, nayo maskini safina ikitupwa huko na huko kwenye maji; ilikuwa ni baada ya gharika kumalizika, ambapo aliona upinde wa mvua kwa mara yake ya kwanza, agano la tumaini, agano la ahadi. Akiisha kupitia dhiki, ndipo akaona ahadi.

45 Hivyo ndivyo unavyoiona ahadi, baada ya kupitia dhiki. Nimelipenda shairi hilo, ama zaburi:

> Je, yanibidi kubebwa nyumbani Mbinguni
> Katika kitanda kizuri cha starehe,
> Wakati wengine walipiga vita wapate kushinda tuzo
> Na kuabiri katika bahari zilizojaa damu?

46 Tunaomba tupate faraja na amani. Mungu hutupa kilicho bora zaidi awezacho kutupatia: majaribu na dhiki. Hizo ni bora kuliko faraja na amani. Faraja zetu ziko tu ng'ambo ya mto.

47 Ilikuwa mpaka wana wa Kiebrania walipolazimishwa kuingia katika tanuri la moto, katika moja ya majaribu yao makali sana, ambapo walimwona Mtu kama Mwana wa Mungu amesimama miongoni mwao. Matatizo yao yalimleta Mwana wa Mungu akiwa amesimama miongoni mwao, katika upepo, kupeperusha mbali ukali wa moto. Bali haikuwa mpaka walipoingia katika moto ndipo Mfariji akatokea.

48 Ilikuwa ni Danieli aliyekuwa amedhamiria moyoni mwake kwamba hatajichafua na mambo ya ulimwengu, na alilazimishwa kupitia majaribu, kama angemwomba Mungu au aende katika tundu la simba. Lakini ilikuwa ni baada ya moto kuwekwa, naye akatupwa katika tundu la simba, ambapo, baada ya hapo, aliona Malaika wa Bwana akisimama katikati yake, akizuia, ile Nguzo kuu ya moto ikisimama kati yake na wale simba. Nao simba hawangeweza kumfikia, kwa sababu alikuwa amepitia majaribu na majaribio na matatizo. Naye alijua kwamba Mungu wake aliweza kumwokoa na hayo.

49 Ilikuwa ni Ibrahimu, akiisha kuona nchi ikiwa tasa, na ukame kuingia, naye Lutu akijitenga na kushuka kwenda kuishi kwa uzuri ulimwenguni. Ilikuwa ni baada ya yeye kusikia

miguguno na vilio vya—vya wachungaji wake, bila ya nyasi kwa ajili ya ng'ombe wake, lakini alidumu katika nchi ambayo Mungu alimpa na kumwambia kukaa kwa muda. Na katika siku hiyo, akiisha kujaribiwa mpaka su—subira yake ikafika mwisho, ilikuwa katika siku hiyo ambapo, baada ya majaribu kuisha, alizungumza uso kwa uso na Elohimu chini ya mwaloni siku hiyo. Ilikuwa ni baada ya kupitia majaribu yake, baada ya kupitia matatizo aliyokuwa amepitia, ambapo Mungu alimtokea katika mfano wa Mwanadamu; akaketi pale na kumwambia alikuwa ameoa na jina la mke wake lilikuwa ni Sara, na kusema mke alimcheka, kwenye hema nyuma Yake. Ilikuwa ni hapo ambapo Ibrahimu alimwita "Elohimu." Ilikuwa ni baada ya majaribu na dhiki.

50 Loo, laiti Kanisa lingaliweza kugutuka leo hii, kutambua kwamba baada ya matatizo na majaribu, na kuchekwa na kudhihakiwa, mambo ambayo Kanisa limepitia, Kanisa la kipentekoste; ndipo tunamwona Mungu miongoni mwetu, akifanya ishara kuu, na maajabu.

> Baada ya mahangaiko na matatizo ya siku,
> Baada ya yote kupita,
> Ndipo tutamwona Yesu hatimaye.
>
> Atakuwa ananingojea,
> Yesu mwenye haki na mwaminifu,
> Juu ya enzi Yake ya kupendeza,
> Atatukaribisha Nyumbani
> Siku itakapomalizika.

Kukiwa kungali mchana, na tufanye kazi.

51 Watu hawa wote mashuhuri, ambao wangechukua sehemu kubwa ya ibada yetu ya asubuhi, kuingilia kutaja hilo. Walipitia majaribu, na kumwona Mungu. Walipitia majaribu, wakaona Malaika. Walipitia majaribu; na funuo, na kuona ishara na maajabu, na kadhalika.

52 Lakini, loo, hakuna mmoja wao aliyeona kile Ayubu alichoona. Watu hao wote, baada ya kuona Malaika, na kumwona Mungu na mambo haya yote, hawakuona chochote cha kuwapa matumaini ng'ambo ya kaburi. Lakini Ayubu aliona ufufuo! Aliona Pasaka. Aliona kitu ambacho hufariji kila moyo. Basi alipokiona, "Laiti maneno yangu yangeandikwa kitabuni! Laiti yangechorwa kwa kalamu ya chuma, mwambani!"

53 Unaona, hilo, kila kitu kilikuwa kimegeuka dhidi yake. Ninii Yake, hata watumishi wake wasingezungumza naye. Mke wake akawa mgeni. Hapo aliketi, juu ya lundo la majivu, jaribio kuu. Nalo kanisa likaja, na kumgeuzia mgongo, kwa siku saba. Wala hakuna mtu wa kumfariji!

54 Ndipo hapana shaka aliona ono la Pasaka, wakati alipolia kwa sauti, "Ninajua Mtetezi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Najua! Laiti maneno yangu

yangechorwa kwa kalamu ya chuma, mwambani, hata maneno yangu yasifutike kamwe, kwa kuwa najua Mtetezi wangu yu hai! Najua! Najua!"

55 Unajua nini, Ayubu? "Najua Mtetezi wangu yu hai." Hivi mlitambua, si tu kwamba kulikuwa na Mtu aliye hai, bali Yeye alikuwa ni Mtetezi wa Ayubu!

56 Loo, Jina la Bwana libarikiwe. Nina furaha sana kwamba mimi ni sehemu ya Pasaka, kwamba mimi ni sehemu ya huo ufufuo! Na sisi ni sehemu yake asubuhi ya leo, kwa sababu ndani yetu unakaa Uzima huo wa ufufuo (yaani, mshiriki) ulioleta Pasaka. "Najua kwamba Mtetezi wangu. . ." Unajua nini? Sibahatishi juu ya hilo; tuna kubahatisha kwingi kupita kiasi siku hizi. "Najua Mtetezi wangu yu hai!" Naam, bwana.

57 Sasa Yeye alikuwa ni kitu gani? Kama aliishi, Yeye alikuwa ni Mtetezi wa Ayubu. "Wangu," binafsi, *wangu,* "Mtetezi wangu yu hai!"

58 Na ni kitu gani kingine unachokijua, Ayubu? Uliona nini katika ono hilo? "Na katika siku za mwisho, Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa mabuu ya ngozi yauharibu mwili wangu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona nafsi yangu. Najua Mtetezi wangu yu hai, na Yeye atasimama juu ya nchi katika siku ya mwisho. Ingawa viuno vyangu viangamie ndani yangu, ingawa mabuu ya ngozi yauharibu mwili wangu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Kupitia hapo lilikuwa ono kubwa kuliko yote.

59 Danieli aliona Malaika. Wana wa Kiebrania walimwona Mwana wa Mungu. Nuhu aliona upinde wa mvua. Ibrahimu alimwona Mungu, uso kwa uso. Bali, Ayubu aliuona ufufuo, Ayubu alitazama mbele. Wazee wote na watakatifu mashuhuri, wa Biblia, waliitazamia siku hiyo; wakiwa na hakikisho, kupitia maono yao, kupitia funuo zao, kwamba kutakuja wakati wa ufufuo.

60 Sasa tunaona kazi kuu zikiendelea. Tunaona nguvu kuu za Mungu. Tunaona mambo makuu ambayo Yeye angeweza kufanya. Usingeweza kuangalia jua na—na kujua ya kwamba si Nguvu za Mungu zinazoleta ulimwengu kulizunguka hilo jua. Usingeweza kuona majira ya kuchipua yakija pasipo kujua kwamba Mungu yupo. Unaweza kuona uponyaji wa macho yaliyopofuka, masikio ya kiziwi, ujue kwamba ni Mungu. Lakini vipi kama hayo ndiyo yote yaliyokuwapo, na baada ya sisi kufa tumekwisha? Lakini ufufuo, Pasaka, loo, huo ndio uliotia muhuri kila kitu ambacho Mungu aliahidi, ulikuwa ni ufufuo.

61 Nao inabidi wawe na kusulubiwa, kabla ya kuwa na ufufuo. Na kabla ya Kanisa kuweza kuona Nguvu zilizofufuka, kabla sijaweza kamwe kuona huduma mpya ikitokea mimi mwenyewe, kabla hujaweza kuingia katika ushirika mpya na Mungu, hapana

budi pawe na kujisulubisha mwenyewe kusudi kuweze kuja ufufuo. Hatuna budi kufa kwa mawazo yetu wenyewe, kufa kwa njia zetu wenyewe, kufa kwa kila kitu kilichotuzunguka, tupitie majaribu na dhiki, ili tuweze kuona ufufuo mpya, Uzima mpya. Kabla ya mwenye dhambi kuweza kufanyika Mkristo, hapana budi kuje mauti, kisha ufufuo.

62 Kabla Ibrahimu kuweza kumwona Elohimu, ilibidi kuwe na miaka ishirini na mitano ya kujaribiwa. Kabla wana wa Kiebrania kuweza kumwona Mwana wa Mungu, ilibidi waingie katika tanuri la moto. Kabla ya Danieli kuweza kumwona Malaika, ilimbidi kuingia katika tundu la simba. Kabla ya Ayubu kuweza kuona ufufuo, ilimbidi kuingia na kupoteza kila kitu alichokuwa nacho; lakini basi, kwa ono, aliona!

63 Na ikiwa Ayubu kwa ono aliweza kusimama imara sana juu ya ahadi, ni zaidi sana vipi sisi tunapaswa kusimama, baada ya Kristo kufufuka kutoka kwa wafu na kufanyika Malimbuko ya Kwanza ya wale waliolala, na kumtuma Roho Mtakatifu kama muhuri wa ahadi, juu yetu, ili sisi pia tupate kuishi. "Kwa sababu ninaishi, nanyi pia mtaishi!" Tukiona Uwepo Wake mkuu miongoni mwetu, ukitenda kazi, ukifanya ishara zile zile na maajabu aliyofanya duniani, ukitupatia matumaini. Nasi tunafikia ufufuo, na kisha kubaki juu ya malundo yetu ya majivu? Hebu tuondoke kwenye lundo la majivu leo hii, tukiwa na ono jipya, pamoja na Nguvu mpya, na azma mpya kwamba tunamwona Mungu katika Nguvu Zake. Tunaona ufufuo wa vitu ukija.

64 Tuko kwenye wakati wa mauti. Tumeketi kwenye milango ya mauti. Mataifa yako kwenye milango ya mauti.

65 Urusi imegundua silaha mpya sasa, kama nyote mlivyosikia kwenye redio na kadhalika. Haiwabidi kuja huku ili kulilipua kwa bomu. Wanaweza tu kuleta kitu kidogo huku, na kuingia miongoni mwa wapelelezi wao, na kububujisha kitu kidogo katika taifa lolote, na kila mtu atapooza kwa saa ishirini na nne. Waje huku na, wakati ukiamka, yupo Mrusi anakupiga teke ubavuni, mlinzi mkubwa wa Kirusi akichukua mamlaka ya nyumba yako, akimbaka mke wako, kuwatupa watoto wako huko nje mtaani, na kuchukua nyumba yako. Wanaweza kufanya hivyo. Wasingepoteza hata kitu kimoja. Wanayo. Hakuna mtu ajuaye kwamba hiyo ni nini. Unaona, kila kitu kikifanya kazi ndani. Sasa wanaweza kutumia hiyo na wasiiogope, kwa sababu hakuna mwingine aliye nayo.

66 Hatujui jinsi itakavyokuja, kile kitakachotukia. Bali tunajua jambo moja, kwamba tuko kwenye lundo la majivu. Taifa, liko kwenye lundo la majivu. Ulimwengu uko kwenye lundo la majivu.

67 Na kwa sababu ulimwengu uko kwenye lundo la majivu, nina furaha sana kwamba Roho wa Mungu anaweza kuja,

nasi tunaweza kusema, "Ninajua Mtetezi wangu yu hai, na katika siku ya mwisho Yeye atasimama juu ya nchi!" Siku moja atakuja! Si ajabu mshairi aliandika:

Alipoishi, alinipenda. Alipokufa, aliniokoa.
Alipozikwa, alipeleka dhambi zangu mbali kabisa.
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele.
Siku moja Yeye yuaja, loo, siku tukufu!

68 Ilihitaji Gethsemane, ya matone ya Damu yakipenya kupitia ngozi Yake, kabla ya hapo. Na ilihitaji maumivu makali ya Kalvari, kabla hakujaweza kuja thibitisho la Mungu wa Milele Ambaye aliweza kuwafufua wafu. Ilihitaji—ilihitaji Gethsemane na Kalvari, kufanya Pasaka. Hakika ilihitaji.

69 Jinsi wale mitume, kwenye asubuhi ile, wakati walipokuwa wamefishwa moyo sana, hata Petro akasema, "Nimefishwa moyo sana, ninaamini nitarudi tu kuvua samaki tena. Nitarudi huko chini. Mimi, mimi nimemwona."

70 Walikuwa na matumaini makubwa, na kuamini na kila kitu, hata ikafikia mahali hapo pakuu pa giza. Mungu alikuwa anafanya nini? Alikuwa anawaleta hao mitume kwenye lundo la majivu. Alikuwa anawaleta mahali ambapo wangekuwa wangethibitishiwa imani yao.

71 Ndipo Petro akasema, "Ni—nimemwona akifanya miujiza mikuu huko chini Galilaya. Lakini, loo, amelala huko, amekufa, na baridi, kaburini! Ninaamini nitateremka tu baharini asubuhi ya leo na kutupa wavu wangu, na niende tu kuvua samaki. Labda ninaweza kuangalia huko ng'ambo ya bahari, nami nitajua. Ninakumbuka kumwona wakati alipotungojea ufukoni. Ninaamini nitaenda tu huko chini."

72 Nao mitume wakasema, "Unajua nini? Ninaamini nitaandamana tu nawe." Loo, walikuwa bluu. Walikuwa wamelia mpaka macho yao yakavimba.

73 Jinsi tunavyojua kupitia sehemu hizo! Jinsi tunavyojua! Sote tunafahamu mambo hayo.

74 Ninakumbuka wakati nilipomlaza mpendwa mmoja huko kaburini, huko juu ya kilima huko, kunakoitwa Mashariki, ama Makaburi ya Walnut Ridge. Jinsi nilivyomlaza mtoto mchanga kule! Nami ningelia mkononi mwa mamangu, mpaka, nililia mpaka sikuweza kulia tena. Nilikuwa nimefanya chochote nilichokijua. Hata, nikachukua bunduki, kujaribu kujiua, nilikuwa katika wakati mgumu sana. Basi ilikuwa kwenye wakati huo, katika chumba hicho kidogo huko juu, nikiwa nimepiga magoti, ndipo Mbingu zilifunguka, nami nikamwona amesimama pale katika fahari ya kutokupatikana na mauti. Ilikuwa kwenye wakati huo ambapo nilihisi mikono yake ikizunguka mabega yangu, kasema, "Bill, huelewi. Tuko bora kabisa kuliko ninyi."

75 Mnaona, inahitaji kusulubiwa. Inahitaji kupondwa kwa ua, ili kutoa manukato kutoka kwake. Inahitaji kupondwa kwa uhai, kupata kilicho chema zaidi chake kilichoko. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Yesu apondwe, ili kuleta kile Yeye alichokuwa. Asingeweza kusimama mbele ya kusulubiwa na kusema, "Mamlaka yote Mbinguni na duniani nimepewa mkononi Mwangu." Lakini baada ya kusulubiwa, angeweza kusimama na kusema, "Mamlaka yote Mbinguni na duniani nimepewa mkononi Mwangu!" Lakini ilifanya nini? Ilihitaji kusulubiwa kwanza.

76 Ilihitaji kupondwa na kufishwa moyo kwa mitume. Walikuwa wamemwona Mwokozi wao, Yule waliyempenda, na kumwona hata akifufuka kutoka kwa wafu kutoka—kutoka kaburini. Walikuwa wamemwona akifanya hayo. Na halafu kuwazia, "Yule pale amelala, baridi, kaburini, Mwenyewe, asubuhi ya leo." Ilihitaji . . .

77 Wale watu waliokuwa wamemwona akifungua macho ya vipofu, walikuwa wamemwona akisimama pale na kutambua mawazo hasa katika mioyo ya watu, "Alijuaje," wangesema, "kwamba hao walikuwa wanamjia? Alijuaje? Ni kwa nini hakumjua Yuda, Yuda ange—angemsaliti? Ni kwa nini hakujua hao askari walikuwa wanapanda juu milimani huko, wakiwa na marungu na panga na kila kitu, kumshika Yeye, kama angeweza kutambua mawazo yao?"

78 Mnaona, ibilisi alikuwa anafanya kazi, akiwaweka kwenye lundo la majivu, kwa kuwa walitaka kuwapa ushuhuda wa "najua." (Sio "Nadhani" ama "labda ni hivyo.") "Najua! Najua!"

79 Basi kumbuka, majaribu hayo yanaletwa juu yako vivyo hivyo, ili kwamba usije ukasema, "Vema, labda Hili ni kweli, labda Maandiko ni ya kweli, labda uponyaji wa Kiungu ni wa kweli, labda Roho Mtakatifu ni wa kweli." Bali wakati unapopokea ujuzi huo na kutoka kwenye lundo hilo la majivu, na upate ufunuo wa Mungu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaweza kupiga makelele, "Najua Mtetezi wangu yu hai, kwa sababu anaishi ndani yangu!"

80 Petro alisema, "Nitaenda nivue samaki." Mitume wakasema, "Naamini nitaandamana tu nawe." Na hapo walikuwa kwenye lundo lao la majivu, huko chini katikati ya bahari, na shida ikiendelea jinsi ilivyokuwa. Na ninaweza kumsikia mmoja wao akisema, "Loo, ingewezaje kutukia, Petro? Ingewezaje kuwa kitu kama hicho kwamba Mtu kama huyo angeweza kufa? Angewezaje Yeye kutiwa kaburini jinsi alivyotiwa? Angewezaje Yeye kusimama kuwaacha wamtemee mate usoni na kung'oa ndevu zake, kuweka ile taji kichwani Mwake? Angewezaje Yeye kufanya hivyo, loo, na bado awe ni Mungu? Kamwe siwezi kuelewa." Loo, ni sikitiko la jinsi gani!

81 Ndipo mara ghafla, wakaangalia ufukoni, ufunuo wa aina ile ile tu kama alioupata Ayubu, hapo waliona kile Ayubu alichoona miaka elfu nne kabla. Huyo hapo alisimama Mtetezi, yu hai na mpya, amesimama ufukoni. Na moto uliotengenezwa, na samaki kupikwa juu yake namna hiyo, kisha akasema, akawaalika.

> Yesu anayo meza iliyoandaliwa
> Ambapo watakatifu wa Mungu wanalishwa,
> Anawaalika watu Wake walioteuliwa "Njoni mle;"
> Kwa mana Yake Yeye hutulisha
> Na kutupa kila haja yetu;
> Loo, ni tamu kula pamoja na Yesu wakati wote!

Jinsi tunavyoweza kuwazia hilo, jinsi ambavyo ilihitaji mambo hayo makuu!

82 Jinsi ambavyo...Mtume Paulo, yule mtume mashuhuri aliyekuwa amepitia wakati wake wa shida wakati aliposhuhudia kifo cha Stefano; na kuona maskini uso wake ukiangalia kuelekea Mbinguni, huku mawe yakimpiga usoni, ndipo akaangalia juu na akasema, "Naona Mbingu zimefunguka. Namwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu." Akasema, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii." Huku Paulo amebeba nguo, jambo lililokuwa limemtia kwenye lundo la majivu kwa majuma baada ya majuma, akitembea huku na huko; hata, akili zake zilivurugika, mpaka alikuwa njiani kwenda huko Dameski, kujaribu kupigania njia ya kutokea, kama mtu anayeenda kwenye chupa ya wiski, kujaribu kuzamisha huzuni zake.

83 Alikuwa katikati ya hayo, wakati ilipokuja Sauti kutoka Mbinguni, Nuru kuu inayong'aa ikasema, "Sauli, Sauli, mbona unanitesa Mimi?" Akamwona. Alimtambua, kwamba Yeye alikuwa ni Yesu aliyefufuka, Yule aliyekuwa ameshuhudia akifa, akafufuka tena.

84 Loo, ninaweza kukumbuka maisha yangu mwenyewe, barabarani nikielekea kuangamia, niliposikia Sauti tamu, "Mimi ni Yesu. Nilikuwa nimekufa, ni hai hata milele. Kwa sababu ninaishi, unaweza kuishi pia." Tangu wakati huo, nikiweka mkono wangu ndani ya Wake, nimemtumainia Yeye kupitia sehemu zenye giza. Nyakati zikija ambapo siwezi kuona, ni njia gani ninaelekea, ningali ninamtumainia Yeye.

85 Kila Mkristo mwaminio hana budi kusukumwa aingie katika majaribu hayo. Kila Mkristo mwaminio hana budi kuwekwa juu ya lundo la majivu, ili kwamba aweze kutokea na ujuzi, "Najua Mtetezi wangu yu hai!"

86 Hatuji hapa asubuhi ya leo kuketi tu na kuongea kuhusu swala fulani la kihistoria, ambalo ni kweli kabisa, bali tunakuja hapa tukiwa na ushuhuda asubuhi ya leo, "Najua kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Ninalijua kupita shaka lolote!

Ninajua ya kwamba Yeye alifufuka kutoka kwa wafu, na yuaishi ndani yangu leo hii. Yeye ni wangu na mimi ni Wake. Mimi ni mrithi pamoja na Yeye, katika Ufalme wa Mungu."

87 Pasaka! Pasaka huleta jambo kuu, ufufuo, tumaini jipya. Je, umelipata asubuhi ya leo? Liko moyoni mwako? Je, unajua kwamba Mtetezi wako yu hai, na Yeye hufanya mambo yote kufanya kazi kwa pamoja?

88 Unasema, "Ndugu Branham, nimeketi hapa, nikingojea mstari wa maombi."

89 Mungu anafanya hiyo hasa kwa wema. Ni kwa nini yule mvulana mdogo wa thamani, hivi majuzi, alipigwa na upofu wakati alipozaliwa? Kusudi Mungu apate utukufu na kulivuruga jiji kabisa. Hakika, Mungu anajua kile Yeye anachofanya. Mungu anajua. Na Yeye hutuweka kwenye lundo la majivu, ili kwamba atuonyeshe utukufu Wake.

90 Hivyo basi, asubuhi ya leo ninasema hili, rafiki. Baada ya miaka thelathini na moja ya huduma, baada ya miaka thelathini na moja ya kazi ngumu hudumani, ninataka kutoa ushuhuda wangu kwa hili. Nimeona masikitiko. Nimeona wakati ambapo nimeomba vitu, na kulilia vitu, na kusihi nipate vitu, nikakosa kuvipata. Lakini ikiwa nitamngojea tu Mungu kwa subira, basi ninajua kwamba hufanya kazi hasa kabisa, hutokea vizuri kabisa, hufanya hasa jambo lifaalo.

91 Nilipompoteza mtoto wangu mchanga, maskini Sharon wangu, mimi...hilo ni jambo moja ambalo lilinikwaza. Nikasema, "Hilo linawezaje kuwa kwa ajili ya wema? Hilo linawezaje kuwa kwa ajili ya wema?" Ndipo miezi kadhaa baadaye, nilipomwona amesimama huko katika uzuri wote wa msichana mdogo, akizungumza nami, huku amesimama kando ya maskini lile behewa lililoharibika, pale. Nilijua, kama angaliishi, huenda angeenda njia mbaya. Ilibidi Mungu amchukue angali mdogo na mzuri. Ninajua nitamwona tena. Ninajua nitamwona, ninajua hilo mbali na mashaka yoyote.

92 Ninawaza juu ya mke wangu wa umri wa miaka ishirini na miwili, aliyechukuliwa, akiwa ni msichana tu, mama mchanga pale. Wakati magazeti yakiweka kichwa cha habari hapa, "Mama mchanga, kasisi . . . , amefariki tu," loo, jinsi moyo wangu ulivyohuzunika! Sikujua la kufanya.

93 Lakini leo ninajua yote yalikuwa yanatenda kazi kwa wema kwa ajili yangu. Ninajua uhai ilibidi usagwe, na kupinduliwa, na kubinywa, kufanya kilichokuwa ndani yake, kitoke. Kulikuwa na Branham mwingi sana humo ndani, ilibidi abinywe atoke kabla ya Mungu kuweza kujitambulisha Mwenyewe.

94 Kulikuwa na uwewe mwingi kupita kiasi ndani yako, hata ilibidi Mungu abinye utoke, kupitia majaribu. Na wakati kubinywa huko kulipokuwa kunaendelea, ni kugumu. Lakini baada ya kitambo, anga zinakuwa wazi, ndipo unaona kusudi

la Mungu. Halafu unapaza sauti, "Najua Mtetezi wangu yu hai, na kwenye siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi! Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu!" Majaribu haya madogo na kadhalika ni ya muda tu, nayo yanapita na kutoweka. Bali yanafanywa tu kwa ajili ya wema wako, hebu tukumbuke hilo, ili Mungu apate utukufu.

95 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Ninataka kuuliza, kabla hatujaomba, je, kuna yeyote hapa angependa kukumbukwa katika maombi kabla hatujafunga? Mungu awabariki. Ni wangapi hapa ndani wangesema, "Ninamtaka Mungu, katika majira ya kujaribiwa kwangu sasa, anipe tukio jipya, ili niweze kutokea mpya tena"? Inua mkono wako, useme, "Ninataka—ninataka huu uwe ni ufufuo kwa ajili yangu, Pasaka, kunifufua mimi katika matumaini mapya na nguvu mpya, afya mpya na furaha mpya." Bwana awabariki, watu wangu wapendwa.

96 Loo, Mungu wetu na Mwokozi wetu, tuna shukrani tele Kwako kwa ajili ya Pasaka hii, kwa ajili ya kile inachomaanisha kwa mioyo yetu. Na kwa imani, huko ng'ambo, ng'ambo ya nchi, tunaweza kuona Kuja kwa Bwana, Yesu, wakati anapojiweka Mwenyewe tayari sasa, akivalia mavazi Yake ya kifalme. Na, Kanisa linavaa, Bwana-arusi anavaa vazi Lake la arusi. Kunakaribia kuwa na mkutano mkubwa karibuni sana.

97 Lundo hili la majivu haliwezi kusimama milele. Tunapowasikia watu wakicheka, wakitudhihaki, na kutuita jina hilo la kashfa la "watakatifu wanaojibingisha," na kutudhihaki, na kusema kwamba sisi hata hatuna akili timamu, loo, haliwezi kudumu muda wote, Bwana. Lakini jalia tuwe kama Ayubu, tushikilie ushuhuda wetu, jalia tuwe kama Danieli katika tundu la simba, ama wale wana wa Kiebrania kwenye tanuri la moto, ama Ibrahimu katika safari yake.

98 Tusaidie, Ee Bwana, kusimama waaminifu mpaka tutakapoona jambo hilo kuu likitukia, "Wakati baragumu itakapolia, na wafu katika Kristo watafufuka; sisi tulio hai na tuliosalia tutabadilishwa, katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua, jicho." Ndipo kutatokea ile Pasaka kwa ajili yetu, ambayo Kristo aliifurahia miaka elfu moja mia tisa iliyopita asubuhi ya leo, na akasema, "Kwa sababu Mimi ninaishi, mtaishi pia."

99 "Yesu yuyu huyu, aliyepelekwa juu kutoka miongoni mwetu, atarudi vile vile tu alivyoenda." Tutamwona, hata kila kovu mkononi Mwake na kila alama ya mwiba kichwani Mwake. Tutamwona.

> Loo, nitamjua, nitamjua,
> Na aliyekombolewa nitasimama kando Yake.

100 Naam, Bwana, maskini moyo wangu, wakati huu mwili wangu mnyonge unapoanza kuinama chini ya mzigo, mahangaiko na kazi za mashamba ya mavuno, huduma za umishenari, na mema na mabaya, na kutojali kati ya wahudumu wenye kiburi, na kadhalika, kote mahali hapa, na watu wakibeza, na nguvu za uovu. Lakini, Ee Bwana, siku moja tunakuja kama Eliya, chini kwenye mto; angalia kule, kwenye kila kichaka, limefungwa gari la moto ambalo litatubeba na kutuondoa humu. Tujalie tujue kwamba malundo haya ya majivu ni mapazia tu ya kutuficha na kitu kile kikuu ambacho kiko tu mbele kidogo, ule utukufu mkuu.

101 Jalia tudumu wakweli kama Ayubu, hata tunaweza kumwona, uso kwa uso. Jalia tuwe wakweli kama Bwana wetu alivyokuwa, kama mfano wetu, kwenda Kalvari; pia, tayari kusulubiwa, na kusulubiwa pamoja na Yeye, kusudi kuwe na ufufuo maishani mwetu. Tujalie, Bwana.

102 Jalia, kukiwepo na wenye kubeza hapa, waliokuwa kama Paulo wa kale, ambao wamefanya dhihaka, jalia wapate Pasaka njiani mwao kuenda nyumbani asubuhi ya leo. Tujalie, Bwana.

103 Tunaomba, Bwana, ya kwamba wale walio kwenye lundo la majivu ya maangamizi, lundo la majivu ya ugonjwa, kwamba hii itakuwa ndiyo saa ambayo watakombolewa.

104 Jana usiku, nikizungumza na maskini mwanamke yule kwenye trela, pamoja na mume wake; jinsi ambavyo kule Phoenix, katika hali mahututi, na zile kansa kubwa zikiwa juu yao, na sasa leo hii ni mzima kabisa na mwenye afya. Naye maskini mtoto mchanga aliyekuwa akienda kuondolewa moyo wake, ameketi hapa katika jengo hili asubuhi ya leo, mzima, mwenye afya. Mvulana mdogo kipofu ambaye wakati mmoja alitembea katika giza bila kuona mwanga wa mchana, anatembea leo hii na kuona mwanga wa mchana. Na, Ee, Mungu, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili! Na yote yanatazamia ng’ambo ya pazia, kwenye ile siku kuu ya ufufuo. Tujalie, Baba. Na uwajalie wajue kwamba mambo haya ilibidi yawe hivyo, ili hawa: mvulana mdogo kipofu aweze kuona, ili maskini mtoto aliye na tatizo la moyo aweze kutoa ushuhuda kwa wengine. Mambo haya yote hutenda kazi pamoja kwa wema kwa hao wakupendao Wewe.

105 Yote yamefanywa yawezekane kwetu kwa sababu kulikuwa na Mmoja aliyetii katika majaribu, kulikuwa na Mmoja aliyestahimili majaribu, huyo alikuwa ni Yesu. Yule Ambaye alikuwa mtiifu sana kwa Baba, hata Baba akamfufua asubuhi ya Pasaka, kwa sababu haikuwezekana kwamba ashikiliwe na mauti. “Kwa kuwa sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake kuzimuni.” Kwa kuwa, Yeye alionekana kuwa mwaminifu, siku zote akifanya yale yaliyompendeza Baba.

106 Mungu, tujalie tuwe waaminifu siku zote kwenye wajibu wetu. Haijalishi majaribu yetu ni nini na matatizo yetu, chochote kile, tujalie tuweze kusema, siku zote, "Najua ya kwamba mambo yote hutenda kazi pamoja kwa wema kwa wale wampendao Mungu." Tujalie, Baba.

107 Tunawabariki watu hawa asubuhi ya leo kwa baraka Zako. Wamekuja mapema kutoka kwao, wamekuja maskanini. Wamekuja wapate faraja. Jalia waende nyumbani asubuhi ya leo, huku Nguvu za Roho Mtakatifu zikiwaka mioyoni mwao, wakitembea barabarani kama wale wanaotoka Emau, wakisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, aliponena nasi njiani?" Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

Vema, Ndugu Neville. Na sasa kumbukeni ibada.

108 Hatutakuwa na kadi za maombi asubuhi ya leo, kwa sababu kwamba, tukiwa na kadi za maombi, mradi tu nimeweka watu kusimama hapa namna hii, ningali nitategemea karama hiyo. Inanibidi kuwa na mahali mpaka niweke upande huo, ambapo ninaweza kutoka hapa nje na niweze. . . Ninahofia. Ninaonekana kuhofia, nami ninahofia kuwa nitakosea. Kushindwa vita, si kupoteza mapambano. Patton alishindwa vita vingi, bali kamwe hakupoteza mapambano. Hiyo ni kweli. Nasi tutashindwa vita vingi, pia, bali hatutapoteza mapambano. Nitafanya makosa mengi, bali sitapoteza Huduma. Mungu aliitoa, naye Mungu ataishughulikia. Ni—ni upako. Na sasa ni wakati, ninaamini saa imewadia, nami ninaanza, kwa kuwa ni Pasaka leo hii, ninaenda ku—kuendelea kama nilivyofanya huko nikiombea wagonjwa. Na kama nikiweza. . . Ni upako. Ni jambo fulani halina budi kutukia ndani yangu. Sijauzoea sana. Huja katika njia ambayo, huenda nisiweze kuutambua tu vizuri, bali inanibidi kuzidi kuendelea nao hata niujue kila wakati. Kwa hiyo hii itakuwa ndiyo siku ambayo nitajaribu, kwa neema ya Mungu.

109 Bwana awabariki sasa. Ndugu Neville. Na ibada zitaanza saa tatu u nusu. Ndugu Neville.

*Najua* SWA60-0417s
(I Know)
Mfululizo wa Ujumbe wa Pasaka

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye Jumapili ya Pasaka asubuhi wakati wa mapambazuko, mnamo tarehe 17 Aprili, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org